

UGONJWA WA MAFUA YA KUKU (INFECTIOUS CORYZA OR FOWL CORYZA)

Na Augustino Chengula

Ugonjwa wa kuku ni ugonjwa wa kuambukiza unaoshambulia zaidi mfumo wa juu wa upumuaji kwa kuku na dbaadhi ya ndege wa porini mfano njiwa. Ugonjwa huu unasababishwa na bakteria wanaojulikana kitaalamu kama *Avibacterium paragallinarum* (zamani alitwa *Hemophilus paragallinarum*). Ugonjwa wa mafua ya kuku unaweza kuwapata kuku wa umri wote lakini zaidi wale wa umri wa kati na wakubwa. Aidha unajitokeza zaidi kwa kuku wanaotaga na wale wanaokaribia kutaga mayai na mara chache hujitokeza kwa kuku wa nyama.

Uenezwaji

Ugonjwa huu huenea kutoka kuku mmoja kwenda kwa kuku mwingine au kutoka banda/shamba moja kwenda jingine kwa njia ya kugusana kati ya kuku na kuku au watu wenye wadudu au kwa njia ya hewa kupitia chembe chembe ndogo za vumbi na pia kupitia maji ya kunywa. Uenezwaji kwa njia ya vyombo vya chakula pia unawezekana.

Ugonjwa unaweza ukaanza na kuku wachache huku ukienea taratibu na kuishia na kuku wachache au ukaenea kwa kasi na kushambulia kuku wengi. Ugonjwa unapatikana sehemu mbalimbali duniani na baadhi ya maeneo hujitokeza mara kwa mara. Kwa Tanzania ugonjwa huu hujitokeza hasa kuanzia mwezi wa tano hadi wa nane.

Dalili za Mafua ya kuku

Kufuatia maambuzi ya ugonjwa huu, dalili huanza kujionyesha tangu siku ya 1 hadi ya 4. Dalili zake ni kama ifuatavyo:

-Kwa **ugonjwa wenye madhara madogo**, dalili zinazoweza kuonekana ni kuzubaa, kuchuruzika mafua mepesi na mara chache kuvimba uso kwa kiasi kidogo.

-Wakati ule **ugonjwa mkali** hujionyesha kwa kuvimba kwa kiasi kikubwa maeneo ya masikiona macho pamoja na uwepo wa maji kwenye nyama zinazozunguka maeneo ya macho inayopelekea kufumba kwa jicho moja au yote.



Kutoa makamasi mazito yaliyochanganyika na usaha puani na mdomoni, vigubiko vya macho hushikana kwa ute mzito ambao huonekana pia ndani ya macho. Kwa kuku dume uvimbe unaweza kwenda hadi kwenye upanga/ndevu. Uvimbe huwa mkubwa kati ya siku ya 10-14.



-Dalili nyingine ni pamoja na kukohoa, kupumua kwa shida kunakosababisha watoe sauti ya mkwaruzo (kukoroma), kuku kutoa machozi, kupungua kwa hamu ya kula kunakowapelekea kushusha uzalishaji (ukuaji na utagaji wa mayai), kuharisha pia kunaweza kutokea, kudhoofika na hatimaye kufa. Utagaji wa mayayi hushuka kwa asilimia kuanzia 14 hadi 40.

Kuku akipasuliwa

-Utando mwepesi au mzito ndani ya pua, macho na masikio wenye rangi ya njano

-Uvimbe wenye maji maji maeneo ya usoni, upanga/ndevu, na upande wa chini wa shingo

-Uwepo wa wekundu na ukahawia au uchafu mweupe ndani ya ngozi inayofunika jicho

-Uwepo wa rangi nyekundu kwenye kuta za koromeo la juu na ute mzito ndani yake

-Mara chache mapafu nayo huathirika

Magonjwa yanayofanana na Mafua ya kuku

-Kipindupindu cha kuku (Fowl cholera)

-Kideri/mdondo

-Mafua makali ya ndege

-Kolibasilosisi (Colibasillosis)

Utambuzi

-Utambuzi hufanywa kwa kutumia dalili za ugonjwa kabla na baada ya kumpasua, na kwenye maabara hutumia darubini kuangalia wadudu baada ya kufanya Gram stain. Lakini pia njia za kibiochemikali pamoja na PCR zinaweza kutumika kubaini bakteria wa ugonjwa huu.

Kupana na ugonjwa wa mafua ya kuku

Tiba- Tiba ipo na inafanya kazi endapo taratibu za matibabu zikifuatwa kikamilifu, madawa ni Sulphathiozole, streptomycin na tetracycline kwa muda wa siku 7.

Kinga- Maeneo ambapo ugonjwa upo muda wote wa mwaka, kuku wachanjwe kwa kutumia chanjo mfu (bacterin). Chanjo ifanyike mara mbili kwa tofauti ya wiki 3 huku chanjo ya kwanza ikifanyika kuku wakiwa na wiki 17.

Epuka kuingiza kuku wapya kutoka mashamba yenye ugonjwa hasa kuchanganya na kuku wa siku moja au wale wazee. Njia nzuri ya kuupoteza ugonjwa huu hasa maeneo yale ambao haupatikani kipindi chote cha mwaka ni kuwaondoa kuku wote wanaobakia mara baada ya ugonjwa. Safisha mabanda vizuri kwa sabuni ya kuua wadudu (disinfectant) na kuacha mabanda bila kuku kwa muda angalau wa wiki mbili kabla hujaingiza kuku wengine. Kuku wapya utakao waleta hakikisha wanatoka shamba linalofuata kanuni za uzuiaji wa magonjwa vizuri na hakuna taarifa ya magonjwa hatari ya kuku.

MAREJEO

- 1.. The Merck Veterinary Manual, 2000. Infectious Coryza, Eighth edition
2. ECTAD, 2010. Picture book of Infectious Poultry Diseases. ECTAD Southern Africa
3. Poultry Hub, TYPES OF DISEASE >INFECTIOUS CORYZA,
<http://www.poultryhub.org/health/disease/types-of-disease/infectious-coryza/>
4. Atlas of Avian Diseases, Infectious coryza, Cornell University College of Veterinary Medicine, 2012. <http://partnersah.vet.cornell.edu/avian-atlas/search/disease/480>